

Ujauzito na

Chanjo za COVID-19

Jilinde wewe pamoja na mtoto wako, pata chanjo ya COVID-19.

**Je, una ujauzito au umejifungua hivi majuzi?
Hiki ndicho unapaswa kujua na kupata chanjo ya COVID-19.**

Kwanini nipate chanjo?

- Wagonjwa wajawazito na waliokuwa wajawazito hivi majuzi wana uwezekano mkubwa wa kuugua sana kutokana na COVID-19
- Chanjo ni salama
- Chanjo inapendekezwa na CDC, ACOG* na SMFM*
- Kupata chanjo ya COVID-19 kunaweza kukuinga kutokana na magonjwa makali yanayosababishwa na COVID-19 na kulinda afya ya mtoto wako



Wakati unapokea chanjo yako ya COVID-19, unaweza pia kupokea:

- Chanjo yako ya homa
- Chanjo yako ya Tdap

Ninanyonyesha Je, mtoto wangu yuko salama ikiwa nitapata chanjo?

Ripoti zinaonyesha akina mama wanaonyonyesha na ambao wamepokea chanjo hiyo wana kingamwili za ulinzi katika maziwa yao, ambayo inaweza kutoa kinga ya ziada kwa mtoto.

*Vituo vya Kudhibiti na Kuzuia Magonjwa (Centers for Disease Control and Prevention), Chuo cha Amerika cha Wataalam wa Uzazi na Wanajinakolojia (the

Ni nini kitafanyika ikiwa nitapatikana kuwa na COVID-19 wakati nina ujauzito?

Unaweza kuwa na:

- Kuongezeka kwa hatari ya shida za kiasya
- Uhitaji wa msaada mkubwa wa oksijeni
- Uhitaji wa kupelekwa katika kitengo cha ICU kwa haraka
- Wagonjwa wanaoambukizwa COVID-19 wakati wa ujauzito wana uwezekano mkubwa wa kuzaa mapema na watoto wao wana uwezekano wa kuwa na kasoro.

Mapendekezo ya Chanjo

Chanjo ya COVID-19 inapendekezwa kwa watu wote ambao:

- Wana ujauzito?
- Wananyonyesha
- Wanajaribu kuwa na ujauzito
- Wanaweza kuwa na uiauzito

Ninapanga kuwa na ujauzito. Je, ninapaswa kupata chanjo ya COVID-19?

Hakuna ushahidi wowote kwamba chanjo yoyote, ikijumuisha chanjo ya COVID-19, husababisha shida za uzazi.



Kentucky Public Health
Prevent. Promote. Protect.

Ili kupata chanjo karibu nawe, tembelea
vaccine.ky.gov